

## KISWAHILI

**Jibu maswali yote kwenye nafasiulizoachiwawazibaada ya kila swali.**

**A. UFAHAMU:**

**Soma makalayafuatayokishaujibu maswali yanayofuatia.** Michuano ya mechi ya kutafutatimubingwa katika mchezowakabumbubaraniAfrikamwaka wa 2004 ilifanyikanchini Tunisia, iliyojanibu ya Afrikakaskazini. Mjimkuuwa Tunisia, Tunis ulikuwamahali pa kilaaina za **shamrashamra** kwa wenyeji na wageni. Michezo hii huandaliwabaada ya miaka miwili nahuchukuasikukadham**tawalia** ingawa panaweza kuwa na siku za mapumziko. Mjiulinadhifishwananyugaziliandaliwa kwa michuanohiyo. Michuano hii ilishirikisatimukumina sita. Mataifa yote thelathinina sita hayakushiriki yote kwa sababu ya kushindwa au nyinginezo.

Timuzinazolingia katika kinyang'anyirohichohupatikanabaada ya mashindano ya mchujo. Hapo, nchihuchezamechi za nyumbani nazile za ugenini. Timuhizihuwa katika makunditofauti.Washindi kutoka kilakikundi hushirikimkondowapiliambaohuwa wa mchujo wa mechi za nyumbani na ugenini.

Madhumuni ya mechi hizi aghalabuhuwamengi:

kuletaumojamiongonimwamataifawashiriki, kuburudisha, kuletaufahamikiano katika Nyanja za utamaduni, mitindo ya mavazi, vyakulanakadhalika. Mara nyinginenimawindo ya timu kutoka njehasamataifa ya Ulayakutafutawachezajistadi. Miongonimwawachezajiwalioshiriki, wamowengi wanaochezeatimu za nchi za Ulayaambakowanapewafulusinyingi.Jambo hili hupokonyabara la Afrikatalantazake! Ukweli ni kwamba vilabuvyanjehuwalipawachezajivizuri na vinausimamizi bora kulikoilivyo katika nchinyingibaraniAfrika.

Usimamizimbayahufanyahali ya michezokuzorota katika nchi za Afrika.Kuepukananajambo hili lazima mashinanikuwe na vilabuvinyosaidiwa na kamai au shirikalinalohusinana na mchezohuu. Piani bora kuazishakambi za vijanachipukiziilikupatawachezajiwatokaoinuatimu ya taifa.

Michezo hii ya baraniAfrikahuwakigezo cha ujuzinaumahiri wa wachezaji katika kusakatakabumbu. Aghalabuwachezajihutuzwakutokananajuhudizao katika ngazi hii ya **kilele**. Kwa mfano, mchezajialiyefungamabaomengi au aliyeonyeshaumahiriwakipekee katika michuanohiyohutuzwamedali.

Michuano hii huiletanchiandalizifaidanyingi. Kwa mfano, kuborekakwanjia za mawasiliano, kupatawageni wanaotaliimiongonimwa mengine. Baadhi ya

wagenihasamakochahuja kufanya ujasusi juu ya miambawabara hili ambaowatamenyananao katika michuano ya kuwaniakombe la duniainayofanyikabaada ya kilamiakaminne.

Nidhamunijambolinalotiliwamaanani sana katika shughuli hiyo. Wakatimwingine kwa sababu kadha wa kadha za kinidhamu, mchezaji wa timu fulani huwezakurudishwa nyumbani. Miongonimwamakosa haya ni kutumia dawa za kuongezeamisulinguvu, kupigana na ulevi.

Mwishowakinyang'anyirohiki Tunisia iliibukatimubingwa na ilitunukiwakombe, medali na kitita cha pesa.

### 1. **Maswali:**

(i) Taja faida tatu ambazo nchiandalizi ya mechi hizi za kandandahupata. (alama 2)

(ii) Kwa nini mchezaji hufukuzwa katika kampi? (alama 2)

(iii) Sababu zipi hufanyawageni kujakutazamamichezo hii? (alama 2)

(iv) Timu inayoibukabingwahupewa nini? (alama 2)

(v) Eleza maneno haya kamayalivyotumiwa katika taarifa. (alama 4)

(a) Fulusinyingi –

(b) Kabumbu –

(c) Shamrashamra –

(d) Kuwania –

### 2. **SARUFI**

(a) Sautini nini? (alama 2)

(b) Kuna sauti aina ngapi? Zitaje. (alama 2)

(c) (i) Silabi ni nini?

(ii) Neno hili linasilabigani?(labda) –

(iii) Andika sentensi hii KKII

(d) Akifishasentensi hii:

Ann: Musa musaunaitwamusa na nani Ann na mama (alama 3)

(e) (i) Eleza maana ya mofimu (alama 1)

(ii) Neno hili linamofimungapi? (mwanahewa) (alama 1)

(iii) Mofimuzikongapi? Andika mfanowakilamofimu. (alama 1)

(f) Hizininomino za ainagani? (alama 4)

(i) ‘Oduor –

(ii) ‘Miti –

(iii) ‘Mchanga –

(iv) ‘Jeshi–

(g) Fafanua vivumishivilivyopigwamstari. (alama 3)

(i) Mtotomwerevuamefuzu

(ii) Mahaliganihapa –

(iii) Baba yangunihuyu -

(h) Tumiakihusishikifaacho kutoka jedwalikujazapengo (kumbe, ala, alhamdulillah)

(alama 1)

Nilikufikiria kuwa Rafikimwema \_\_\_\_\_ weweniaduimkubwa.

(i) Jazaviambishivifaavyo:-

(alama 4)

(i) Huyundi\_\_ aliye \_\_\_ chunguzaulipotupamawe.

(ii) Huund\_\_mkuki \_\_li\_\_rushwa.

(J) Pambanuasentensi hii kwanjia ya mstari.

Mwanafunzimwewevuhusomavitabuvingi.

(alama 2)

(k) Andika katika hali ya udogo

Nyumbayangundogolakiniinawapangajiwengi.

(alama 2)

### 3. ISIMU JAMII (ALAMA 6)

(a) Eleza maana ya lugha.

(alama 3)

(b) Toa sifa tano za lugha .

(alama 4)

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

### 4. FASIHI SIMULIZI (ALAMA 6)

(a) (i) Eleza maana ya kitendawili.

(alama 2)

(ii) Andika dhimazozotenne za vitendawili. (alama 4)